*Kioo cha Lugha, Juz. 21(1), 1-20*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam* DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v21i1.1

# Uainishaji wa Ngeli za Nomino za Kivunjo Kimofolojia

*Ruth N. Shao[1] na Salome J. Kotira[2]*

## Ikisiri

Makala hii inashughulikia uainishaji wa ngeli za nomino katika lugha ya Kivunjo na kubainisha idadi yake kimofolojia. Ili kutimiza malengo haya, mbinu ya usampulishaji nasibu pangilifu imetumika katika kuwateua watoataarifa ambao ni wazungumzaji wa Kivunjo. Data zimekusanywa kwa kutumia hojaji, usaili na ushuhudiaji. Mkabala mseto, yaani wa kimaelezo na kiidadi umetumika katika kuwasilisha na kuchanganua data za utafiti huu. Aidha, utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Mofolojia Asilia (NMA) iliyopendekezwa na Dressler (1985) na Wurzel (1987). Pamoja na nadharia hii, mkabala wa Viambishi Awali vya Nomino umetumika kubainisha viambishi ngeli vya nomino katika misingi ya umoja na wingi. Hivyo, kwa kutumia Mkabala wa Viambishi Awali vya Nomino matokeo ya utafiti huu yamebainisha kuwa lugha ya Kivunjo ina ngeli 18.

## 1.0 Utangulizi

Kivunjo ni lugha ya Kibantu inayozungumzwa katika maeneo ya Kaskazini Mashariki mwa Tanzania, mkoani Kilimanjaro. Wazungumzaji wa lugha hii wanaishi katika miteremko ya Mlima Kilimanjaro katika wilaya ya Moshi Vijijini. Wilaya hii iko katikati ya wilaya za Hai na Rombo. Hii ina maana kwamba wazungumzaji wa lugha ya Kivunjo ni wale waishio maeneo ya Kirua, Kilema, Mwika, Mamba na Marangu. Aidha, lugha ya Kivunjo inakaribiana sana na lugha nyingine, kama vile Kirombo, Kikibosho, Kimachame na Kiuru (Elisifa, 2008).

Kivunjo ni mojawapo ya lugha za Kibantu ambazo hazijafanyiwa utafiti katika kipengele changeli[3] za nomino. Kwa kiasi fulani, lugha hii imeshughulikiwa katika baadhi ya vipengele. Kwa mfano, Moshi (1976) amefanya utafiti katika

[1] Mhadhiri na Mtafiti, Chuo Kikuu cha Hamburg, Ujerumani. Baruapepe: ruth.ndekiro.shao@uni-hamburg.de

[2] Mhadhiri, Idara ya Lugha ya Kiswahili na Isimu, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania. Baruapepe: kotira.salome@udsm.ac.tz

[3] *Aidha*, kuhusu dhana ya "ngeli" Kapinga (1983) na Kihore na *wenzie* (2003:94) wanaeleza kuwa "ngeli" ni neno kutoka lugha ya Kihaya, ***engeli*** likiwa na maana ya aina ya vitu. Kwa mantiki hiyo, istilahi ngeli katika Kiswahili inatumika kwa maana ya aina za nomino katika lugha.

Kivunjo kuhusu ulinganisho wa vikundi nomino vya Kiswahili na vya Kivunjo, Makule (2006) amefanya utafiti katika Kivunjo kuhusu mofimu za ukanushi. Naye Elisifa (2008) amefanya utafiti juu ya motisha katika ujifunzaji Kivunjo kama lugha ya pili. Kadhalika, Kyara (2010) amefanya utafiti kuhusu kirai nomino katika Kivunjo, Kombe (2010) amefanya utafiti kuhusu muundo wa kishazi tegemezi katika Kivunjo na John (2011) amefanya utafiti kuhusu nafasi ya viarudhi katika lugha ya Kivunjo, ambapo alichunguza uamilifu wa toni katika irabu ndefu na fupi. Japokuwa lugha za Kibantu zina mfumo wa ngeli, kuna tofauti fulani zinazojitokeza miongoni mwa lugha hizo (Maho, 1999). Hata hivyo, hakuna utafiti wowote uliofanyika kuhusu ngeli za nomino katika lugha ya Kivunjo. Kwa hakika, hatujui Kivunjo kina ngeli ngapi. Hivyo, utafiti huu unakusudia kuchunguza na kuainisha ngeli za nomino katika Kivunjo ili kuziba pengo la kimaarifa ambalo lipo katika suala la ngeli.

Mfumo wa ngeli ni sifa mojawapo ya kimuundo ya lugha za Kibantu ambapo nomino zinapangwa katika makundi kwa kuzingatia kigezo fulani. Kutokana na nomino za lugha za Kibantu kuwa na sifa ya mfumo wa ngeli, wataalamu mbalimbali wamezipanga katika makundi ambayo kitaaluma yanaitwa ngeli. Kuna wataalamu waliowahi kufanya utafiti juu ya "ngeli" katika lugha mbalimbali. Miongoni mwao ni pamoja na Polome (1976) na Kihore na wenzie (2003) ambao wametumia kigezo cha kimofolojia katika uainishaji wa ngeli za nomino za Kiswahili. Kwa kutumia kigezo cha kimofolojia, Polome (1976) na Kihore na wenzie (2003) wameainisha ngeli 18 za Kiswahili. Naye Kahigi (2005) kwa kutumia Mkabala wa Viambishi Awali vya nomino ameainisha ngeli za nomino 18 za lugha ya Kisumbwa. Aidha, Mutaka na Tamanji (2000:150) wanaeleza kuwa idadi ya ngeli za nomino za lugha za Kibantu inatofautiana kutoka lugha moja hadi nyingine. Hali hii inatokana na kuwa lugha za Kibantu zina asili ya mfumo wa Mame-Bantu[4] ambapo kwa ujumla kuna ngeli kati ya 18 hadi 20. Maho (1999: 54) anaeleza kuwa ngeli za nomino katika lugha za Kibantu zinaanzia 10 hadi 19. Kwa mfano, Kisukuma kina ngeli 18 na Kilwena kina ngeli 15. Tofauti hii ipo pia katika lugha nyingine za Kibantu. Kwa mfano, Besha (1985: 65) anaonesha kuwa Kishambala kina ngeli 17 ilhali Kihore na wenzake (2003: 98) wanaonesha kuwa Kiswahili kina ngeli 18. Lugha nyingine na msimamo wa wataalamu kuhusu idadi ya ngeli katika lugha hizo ni kama ifuatavyo: Kiruri kina ngeli 20 (Massamba, 1995), Kisumbwa kina ngeli 18 (Kahigi, 2005), Kinyambo kina ngeli 18 (Rugemarira, 2005) na Kikagulu kina ngeli 18 (Petzell, 2008). Kutokana na idadi ya ngeli katika lugha za Kibantu kutofautiana, tumeona ni muhimu kufanya utafiti zaidi ili kujua hali ikoje katika lugha ya Kivunjo. Hivyo, utafiti huu umekusudia kuchunguza ngeli za nomino za Kivunjo.

[4] Mame-Bantu ni lugha ya 'kufikirika' ambayo inadhaniwa kuwa ndiyo iliyozaa lugha nyingine za Kibantu.

Kigezo kilichotumika katika kuanisha ngeli za nomino za Kivunjo katika utafiti huu ni cha kimofolojia. Katika kigezo hiki, makundi ya nomino yanapewa namba, utaratibu ambao uliasisiwa na Bleek (1869). Kigezo hiki kiliwahi kutumiwa na wataalamu waliotajwa hapo awali ikiwa ni pamoja na Polome (1976) na Kihore na wenzake (2003). Hivyo, uanishaji wa ngeli za nomino kwa kutumia kigezo cha kimofolojia umetuwezesha kujua idadi ya ngeli za nomino katika lugha ya Kivunjo.

Nomino za Kibantu zina miundo ya aina mbalimbali. Kwa mfano, kwa mujibu wa Katushemererwe na Hanneforth (2010), katika lugha ya Runyakita nomino inaundwa kwa shina na kiambishi ambacho mara nyingi huwa ni cha awali. Uambishaji mwishoni mwa shina hutokea katika nomino zilizopatikana kutokana na unyambulishaji wa vitenzi, vivumishi na vielezi, kwa mfano, nomino *omu+shom+i* (kiongozi) imetokana na kitenzi *kushoma* (kuongoza). Nomino hiyo hupangwa katika ngeli ya 1 na 2 inayohusu watu.

Mutaka na Tamanji (2000: 150) wanaeleza miundo ya nomino katika lugha za Kibantu kuwa inaweza kubainishwa kwa namna tatu kama vile: kiambishi awali + shina (KA+Sh), kiambishi awali tangulizi + kiambishi awali + shina (Kbt+KA+Sh) na kiambishi awali fuatizi + kiambishi awali + shina (KAF+KA+Sh). Aidha, Petzell (2008:47) anatofautiana na Mutaka na Tamanji (keshatajwa) kwa kueleza kuwa nomino katika lugha za Kibantu zinaundwa kwa shina na kiambshi awali kimoja au viwili. Anafafanua kwa kueleza kuwa viambishi hivyo ni irabu tangulizi na kiambishi ngeli. Vilevile, Petzell (keshatajwa) anaeleza kuwa IT (irabu tangulizi) ni ya hiari kutokea. Hii ina maana kuwa watumiaji wanaweza waitumie au wasiitumie na bado maana ikaeleweka. Kwa upande wa kiambishi ngeli, anadai ni lazima kitokee ila wakati mwingine kiambishi hicho hutokea kama kapa. Ametumia kanuni ifuatayo kuonesha muundo wa nomino: IT + KNg + Sh (Irabu Tangulizi + Kiambishi Ngeli + Shina).

Mwendamseke (2011:50) anaeleza kuwa miundo iliyooneshwa na wanaisimu Mutaka na Tamanji (2000:150) sio lazima ijitokeze yote kwa kila lugha. Wazo hili ameliimarisha kwa kuonesha uainishaji wa ngeli za nomino katika lugha ya Kibena na kupata ngeli 18. Mwendamseke (keshatajwa) anaeleza kuwa katika ngeli 18 za lugha ya Kibena alizoainisha, muundo wa kiambishi awali tangulizi + kiambishi awali + shina (Kbt+KA+Sh) ndio unaojitokeza zaidi. Pia, anaeleza kuwa nomino za Kibena hazina muundo wa KA+Sh na KAF+KA+Sh bali zina muundo mwingine ambao haukuainishwa na Mutaka na Tamanji (weshatajwa) ambao ni kiambishi awali tangulizi + kiambishi awali fuatizi + kiambishi awali + shina (Kbt+KAF+KA+Sh). Ikumbukwe kuwa, lugha za Kibantu zinatofautiana na kufanana kwa namna fulani. Hivyo, miundo iliyoelezwa inaweza kutokea yote katika lugha fulani au ikatokea michache. Vilevile, kuna uwezekano wa kutokea miundo tofauti kabisa na iliyoelezwa na wanataaluma hao kama alivyoeleza Mwendamseke (2011) kuwa Kibena kina muundo wa nomino ambao haukuelezwa na watangulizi wake, kama vile Mutaka na Tamanji (2000).

Kutokana na tafiti zilizotangulia, imebainika kuwa lugha za Kibantu hufanana katika baadhi ya miundo, idadi na viambishi vya ngeli. Aidha, baadhi ya lugha hutofautiana katika vipengele hivyo. Hii ndiyo sababu ya watafiti wa makala hii kuchunguza muundo wa viambishi ngeli katika lugha ya Kivunjo ili kubainisha viambishi ngeli vya lugha hiyo pamoja na idadi yake kimofolojia.

## 2.0 Msingi wa Kinadharia

Utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Mofolojia Asilia (NMA) na Mkabala wa Viambishi Awali vya Nomino. NMA ilipendekezwa na Dressler (1985) na Wurzel (1987). Nadharia hii inaeleza kuwa kuna uhusiano wa mofimu na maana zake katika neno. Wurzel anakubaliana na Dressler kuwa NMA inachambua uhusiano baina ya umbo na maana. Nadharia hii imeongoza ubainishaji wa mofimu za nomino za lugha ya Kivunjo na maana zake. Kimsingi, tumependekeza NMA ili kutuwezesha kuainisha ngeli za nomino za Kivunjo kwa kubaini viambishi awali vya nomino.

Mkabala wa Viambishi Awali vya Nomino ambao unatumia kigezo cha kimofolojia, ulianzishwa na Bleek (1862) na baadaye kuboreshwa na Meinhof (1899) kama inavyoelezwa na Massamba (1995: 607). Katika mkabala huu, ngeli za nomino zimeainishwa kwa kutumia viambishi awali vya nomino ambapo kila kiambishi kimepewa namba yake kwa sababu kila kimoja kinaunda ngeli tofauti. Katika utafiti huu, Mkabala wa Viambishi Awali vya Nomino ndio umetumika kama msingi wa uainishaji wa ngeli za nomino za Kivunjo kwa kubainisha viambishi ngeli na kuweka bayana idadi ya ngeli za nomino za Kivunjo.

## 3.0 Methodolojia

Utafiti kuhusu makala hii umefanyika Kaskazini Mashariki mwa Tanzania, Mkoani Kilimanjaro katika Wilaya ya Moshi Vijijini. Usampulishaji nasibu pangilifu umetumika katika kupanga umri wa wataoataarifa, ambapo watoataarifa 40 wamehusika katika kutupatia data za utafiti huu. Watoataarifa wote 40 walikuwa wazungumzaji wa Kivunjo wenye umri kati ya miaka 44-74. Watoataarifa wenye umri huo wameteuliwa kwa sababu ndio walioonekana kuwa na umilisi wa lugha ya Kivunjo tofauti na waliokuwa na umri mdogo. Vilevile, data za utafiti huu zimekusanywa kwa njia ya hojaji, usaili na ushuhudiaji. Watoataarifa 30 wameshiriki katika kujaza hojaji ambapo watafiti waliwafuata katika eneo la ofisi ya kijiji walipokuwa wamekusanyika kwa ajili ya mkutano. Watafiti waligawa vikaratasi 40, vikaratasi 30 viliandikwa namba moja mpaka 30 na 10 havikuandikwa chochote. Wale waliochukua vikaratasi vilivyoandikwa namba 1 - 30 ndiyo walioshiriki katika kujaza hojaji. Katika kuchakata hojaji, watafiti waligawa hojaji zilizokuwa na maswali yaliyolenga kupata data kuhusu nomino mbalimbali za Kivunjo katika maumbo yake ya umoja na wingi. Watoataarifa 30 wameshiriki katika zoezi hili ambapo hojaji 28 zilirudishwa

zikiwa zimejazwa. Kwa kutumia njia ya usaili, watafiti wamefanya usaili wa ana kwa ana kwa watoataarifa 10 ambao walichukua vikaratasi vilivyokuwa havijaandikwa kitu. Katika ushuhudiaji, watafiti walienda wilaya ya Moshi vijijini na walishiriki katika mazungumzo mbalimbali na watoataarifa. Kwa kutumia njia ya usaili na ushuhudiaji watafiti walikusudia pia kukusanya data kuhusu nomino mbalimbali za Kivunjo katika maumbo yake ya umoja na wingi.

Njia zote tatu zimewawezesha watafiti kukusanya data nyingi zinazohusu nomino za aina mbalimbali zikionesha maumbo yake ya umoja na wingi. Hivyo, matumizi ya mbinu mbalimbali za ukusanyaji data yamesaidia kupata data za ukweli, sahihi na za kutosha kadiri ya malengo ya utafiti huu. Aidha, mikabala miwili ya uchanganuzi wa data ambayo ni wa kitakwimu na wa kimaelezo imetumika katika uwasilishaji na uchambuzi wa data ya utafiti kuhusu makala hii. Vilevile, data zilizokuwa katika lugha ya Kivunjo zimetafsiriwa na watafiti katika lugha ya Kiswahili.

## 4.0 Matokeo ya Utafiti

Matokeo ya utafiti yamepatikana baada ya uchunguzi na uchambuzi wa data kuhusu nomino mbalimbali za Kivunjo katika maumbo yake ya umoja na wingi. Vilevile, katika utafiti huu imebainika kwamba ngeli za nomino katika lugha ya Kivunjo zinazoainishwa katika maumbo yake ya umoja na wingi zinaakisi msingi wa Nadharia ya Mofolojia Asilia ya Dressler (1985) na Wurzel (1987) unaoeleza kuwa kuna uhusiano wa mofimu na maana zake katika neno. Msingi huu wa NMA sambamba na Mkabala wa Viambishi Awali vya Nomino umewaongoza watafiti katika kuchambua nomino mbalimbali za Kivunjo ili kubaini maumbo yake ya umoja na wingi na namna umbo moja linavyoweza kujitokeza katika alomofu tofauti. Matokeo ya utafiti huu yamebaini kwamba ngeli za lugha ya Kivunjo hazitofautiani sana na za Kiswahili.

### 4.1 Uainishaji Ngeli za Nomino katika Lugha ya Kivunjo kwa Mkabala wa Viambishi Awali vya Nomino

Data za utafiti huu zimedhihirisha kuwa nomino za lugha ya Kivunjo zina miundo ya aina mbili. Muundo wa kwanza ni Irabu Tangulizi + Kiambishi Ngeli + Shina (IT+KNg+Sh) ambao ndio hujitokeza zaidi katika nomino hizo. Muundo wa pili ni Kiambishi Ngeli na Shina (KNg+Sh). Jedwali Na. 1 linaonesha miundo ya ngeli za nomino za Kivunjo kama ifuatavyo;

**Jedwali Na. 1: Miundo ya Nomino za Kivunjo**

| Na. | Miundo | Nomino |
|---|---|---|
| **1** | IT+KNg+Sh | i + m + ana (mtoto mkorofi)<br>IT KNg Sh |
| **2** | KNg+Sh | m + ana (mtoto)<br>KNg Sh |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2013)

Jedwali Na.1 limebainisha miundo miwili ya nomino za Kivunjo ambapo muundo wa kwanza ni Irabu Tangulizi + Kiambishi Ngeli + Shina (IT+KNg+Sh); kwa mfano, nomino “i+m+ana = imana” kwa maana ya (mtoto mkorofi), *i-* imesimama kama irabu tangulizi, *-m-* imesimama kama kiambishi ngeli na *-ana* imesimama kama shina. Vilevile, katika muundo wa pili, nomino “m+ana = mana” kwa maana ya (mtoto), *m-* imesimama kama kiambishi ngeli na *-ana* imesimama kama shina.

Ingawa nomino za Kivunjo zina miundo ya aina mbili, uainishaji wa nomino katika ngeli unazingatia KNg ambacho ndicho kinachoonesha umoja na wingi. Hivyo, kwa mujibu wa uchanganuzi wa data zilizokusanywa uwandani, zifuatazo ni ngeli za nomino za lugha ya Kivunjo. Sehemu hii inafafanua na kuainisha kila ngeli ya nomino kwa kuonesha viambishi ngeli vyake.

Kabla ya kuainisha ngeli za lugha ya Kivunjo kama zilivyobainika katika utafiti huu na kuchambua ngeli moja moja tutaanza kwa kuonesha muhtasari wa uainishaji wa ngeli za Kivunjo kimofolojia katika Jedwali Na. 2:

**Jedwali Na. 2: Ngeli za Lugha ya Kivunjo kwa Mkabala wa Viambishi Awali vya Nomino**

| Na. | Kiambishi ngeli | Mifano | Kifasiri |
|---|---|---|---|
| **1** | m- | Mndu | Mtu |
| **1a** | Ø | Papa | Baba |
| **2** | wa- | Wandu | Watu |
| **2a** | Ø | Papa | Baba |
| **3** | m- | mři | Mti |
| **4** | m- | mři | Miti |
| **5** | i-/ Ø | iyewo, wee | Jino, ziwa |
| **6** | ma- | mayewo, mawee | Meno, maziwa |
| **7** | ki- | Kiliko | Kijiko |
| **8** | shi- | Shiliko | Vijiko |
| **9** | n- | Numba | Nyumba |
| **10** | n- | Numba | Nyumba |
| **11** | u- | Urusu | Uzi |
| **10** | n- | Ndusu | Nyuzi |
| **14** | u- | Uwicho | Ubaya |
| **6** | ma- | Mawicho | Mabaya |
| **15** | ku- | kuřende | Mguu |
| **6** | ma- | mařende | Miguu |
| **15a** | i- | iřema | Kulima |
| **16** | ha- | Handu | Mahali |
| **17** | ku- | Kundu | Mahali |
| **18** | -nyi | kiṟinyi | Chumbani |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2013)

Kama Jedwali Na. 2 linavyoonekana, ngeli za nomino katika lugha ya Kivunjo, kwenye utafiti huu zimeainishwa kwa kutumia kigezo cha kimofolojia, ambapo

viambishi awali vya umoja na wingi ndivyo vimetumika kama msingi wa uainishaji. Pia, tumedokeza kuwa uainishaji wa ngeli katika utafiti huu umetumia njia ya kuhesabu umbo la umoja na umbo la wingi kama ngeli mbili tofauti. Data za Jedwali Na. 2, zinaonesha kuwa kwa kutumia Mkabala wa Vimbishi Awali vya Nomino kwa kuhesabu umbo la umoja na wingi kama ngeli mbili tofauti, lugha ya Kivunjo imebainika kuwa na idadi ya ngeli za nomino 18.

Aidha, imebainika kuwa baadhi ya ngeli zinajirudia kama katika jozi zifuatazo: Ngeli 9/10, 11/10, vilevile Ngeli ya 5/6, 14/6, na 15/6. Katika jozi hizo ngeli ya 10 na ngeli ya 6 zimejirudia, hii ni kwa sababu ngeli ya 9 umoja na ngeli ya 11 umoja zimechukua kiambishi cha wingi katika ngeli ya 10. Ngeli ya 5, 14 na 15 umoja zimechukua kiambishi cha wingi katika ngeli ya 6. Hii inatokana na kufanana kisifa na kimaumbo. Katika kipengele kinachofuata tumechambua ngeli mojamoja za nomino katika lugha ya Kivunjo kama ifuatavyo:

### 4.1.1 Ngeli ya 1 na 2 [m-wa]

Katika lugha ya Kivunjo, ngeli ya 1 umoja inawakilishwa na kiambishi /m-/. Katika mazingira maalumu, mofimu hii ya ngeli ya 1 umoja hujitokeza katika alomofu mbili ambazo ni: {mw-} na {m-}. Ngeli ya 2 wingi inawakilishwa na kiambishi /wa-/ na kiambishi hiki hakina alomofu. Nomino katika ngeli ya 1 na 2 katika Kivunjo zinaoneshwa katika mifano iliyodhihirishwa katika majedwali Na. 3 na Na. 4:

**Jedwali Na. 3: Nomino katika Ngeli ya 1 na 2[m-/ wa-]**

| **Na.** | **Umoja** | | | **Wingi** | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| (a) | m- | fee | 'mzazi' | wa- | fee | 'wazazi' |
| | KNg | Sh | | KNg | Sh | |
| (b) | m- | chili | 'msimamizi' | wa- | chili | 'wasimamizi' |
| | KNg | Sh | | KNg | Sh | |
| (c) | m- | ndu- | 'mtu' | wa- | ndu | 'watu' |
| | KNg | Sh | | KNg | Sh | |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2013)

Kwa kuangalia mifano a-c iliyoainishwa katika Jedwali Na. 3, kiambishi ngeli cha umoja kimewakilishwa na m-, kwa mfano, katika maneno *m-fee*, *m-chili* na *m-ndu* na kiambishi cha wingi kikiwakilishwa na wa- mfano katika neno *wa-fee, wa-chili* na *wa-ndu* ni viambishi ngeli ya 1na 2. Katika mifano hiyo, mofu /mu-/, hujitokeza kama alomofu {m-} baada ya irabu /u/ kudondoshwa katika mazingira ambapo mzizi wa nomino unaanza na konsonanti mbalimbali.

**Jedwali Na. 4: Nomino katika Ngeli ya 1 na 2 [mw-/ wa-]**

| Na. | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| (a) | mw- injilisti 'mwinjilisti'<br>KNg Sh | wa- injilisti 'wainjilisti<br>KNg Sh |
| (b) | mw- ele 'mtakatifu'<br>KNg Sh | wa- ele 'watakatifu'<br>KNg Sh |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2013)

Katika Jedwali Na. 4 mifano a na b umoja, imewakilishwa na kiambishi cha umoja *mw-* huku mifano hiyo ikiwakilishwa na kiambishi cha wingi *wa-*. Mofimu /mu-/ hubadilika kuwa alomofu {mw-}, pale ambapo mzizi wa nomino unaanza na irabu isiyofanana nayo na kusababisha irabu /u/ kubadilika na kuwa kiyeyusho /w/. Kwa mfano, katika Jedwali Na. 4, maneno *mw-ele* na *mw-injilisti*, kiambishi *mw-* ni alomofu ya kiambishi ngeli ya kwanza *mu-*. Kwa maana hiyo, neno la asili lilikuwa *mu-ele* na *mu-injilisti*.

### 4.1.2 Ngeli ya 1a na 2a [Ø na Ø]

Ngeli ya 1a na ya 2a katika lugha ya Kivunjo inawakilishwa na viambishi /Ø/ umoja na /Ø/ wingi. Viambishi vyote viwili havina alomofu. Aidha, ngeli ya 1 na 2 na ngeli ya 1a na 2a zina sifa za kimaumbo na za kimakundi zinazofanana. Kimsingi, ngeli hizi zinawakilisha viumbe hai. Hata hivyo, katika utafiti huu tumeona haja ya kutofautisha ngeli hizi kwani katika lugha ya Kivunjo ngeli ya 1 na 2 inawakilishwa na kiambishi ngeli "m - wa" ilhali ngeli ya 1a na 2a inawakilishwa na kiambishi fiche "Ø - Ø" katika umoja au wingi. Mifano ya nomino zinazoingia katika ngeli hii ni kama zinavyooneshwa katika Jedwali Na. 5:

**Jedwali Na. 5: Nomino katika Ngeli ya 1a na 2a**

| Na. | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| **(a)** | ø - papa 'baba'<br>KNg Sh | **ø - papa 'baba'**<br>**KNg Sh** |
| **(b)** | ø **-** lawutanyi 'shemeji'<br>KNg Sh | **ø - lawutanyi 'shemeji'**<br>**KNg Sh** |
| **(c)** | **ø - mamela 'kilembwe'**<br>**KNg Sh** | **ø - mamela 'kilembwe'**<br>**KNg Sh** |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2013)

Katika Jedwali Na. 5, mofimu /Ø/ huwakilisha nomino za Kivunjo ambazo hazina umbo halisi la umoja na wingi. Kwa mfano, maneno *papa*, *lawutanyi* na *mamela* ambayo ni umoja na wingi hayana kiambishi chochote kinachodhihirika na hivyo kuwa na mofu ø - kama viambishi ngeli vya 1a na 2a ambavyo ni alomofu za viambishi ngeli vya 1 na 2.

### 4.1.3 Ngeli za 3 na 4 [m-m]

Katika lugha ya Kivunjo, ngeli ya 3 umoja inawakilishwa na kiambishi /m-/. Katika mazingira maalumu, mofimu hii hubadilika na hujitokeza katika alomofu mbili tofauti ambazo ni: {mu-} au {m-}. Ngeli ya 4 wingi inawakilishwa na kiambishi /m-/ na mofimu hii ina alomofu mbili tofauti ambazo ni: {mi-} au {m-}. Nomino katika ngeli ya 3 na 4 katika Kivunjo zinaoneshwa katika majedwali Na. 6 na Na. 7:

**Jedwali Na. 6: Nomino katika Ngeli ya 3 na 4 [mu-/mi-]**

| Na. | Umoja | | | | Wingi | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| (a) | i- | mu- | embe | 'embe' | mi- | embe | 'miembe' |
| | IT | KNg | Sh | | KNg | Sh | |
| (b) | i- | mu- | kepe | 'kopo' | mi- | kepe | 'makopo' |
| | IT | KNg | Sh | | KNg | Sh | |
| (c) | i- | mu- | koke | 'mchwa' | mi- | koke | 'mchwa' |
| | IT | KNg | Sh | | KNg | Sh | |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2013)

Mifano a-c iliyoainishwa katika Jedwali Na. 6, inaonesha nomino ambazo zimeundwa na kiambishi ngeli mu- katika umoja na kiambishi ngeli mi- katika wingi. Nomino hizo zimetanguliwa na IT i- katika umbo la umoja. Kwa mfano, maneno *i-mu-embe*, *i-mu-kepe* na *i-mu-koke*, ambayo ni umoja, kiambishi *i-* ni irabu tangulizi, -*mu*- ni kiambishi ngeli ya tatu umoja na -*embe* ni shina la neno. Hata hivyo, majina yanayopatikana katika viambishi [mu-/ mi-] ni machache[5]. Majina mengi yanapatikana katika viambishi vya [m-/ m-] kama mfano unavyoonesha katika Jedwali Na. 7:

**Jedwali Na. 7: Nomino katika Ngeli ya 3 na 4 [m-/ m-]**

| Na. | Umoja | | | Wingi | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| (a) | m- | ṙi | 'mti' | m- | ṙi | 'mti' |
| | KNg | Sh | | KNg | Sh | |
| (b) | m- | tsu | 'moshi' | m- | tsu | 'moshi' |
| | KNg | Sh | | KNg | Sh | |
| (c) | m- | tsiri | 'mkaa' | m- | tsiri | 'mkaa' |
| | KNg | Sh | | KNg | Sh | |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2013)

Katika Mifano iliyooneshwa kwenye Jedwali na. 7 hapo juu, mofimu /mu-/, hubadilika na kuwa alomofu {m-} baada ya irabu /u/ kudondoshwa katika

[5] Hii ipo pia katika lugha ya Kiswahili, haya ni mabadiliko yaliyotokea kwa sababu ya urahisishaji katika matamshi, ambapo irabu u imedondoshwa kutoka katika umbo la ndani /mu/.

mazingira ambapo mzizi wa nomino unaanza na konsonanti mbalimbali. Kwa mfano, maneno *m-ri*, *m-tsu* na *m-tsiri* ambayo ni umoja na wingi yamebeba viambishi *m-/m-* ambavyo ni viambishi ngeli ya 3 na 4 kwa sababu yana kiambishi *m-* kabla ya shina la neno ambacho ndicho kiambishi ngeli.

### 4.1.4 Ngeli ya 5 na 6 [i-/ Ø na ma-]

Katika lugha ya Kivunjo, ngeli ya 5 umoja inawakilishwa na kiambishi / i-/. Katika mazingira maalumu, kiambishi hiki hubadilika na hujitokeza katika alomofu mbili tofauti ambazo ni: { i-}, au { Ø-}. Ngeli ya 6 wingi inawakilishwa na kiambishi /ma-/ na mofimu hii haina alomofu. Nomino katika ngeli ya 5 na 6 katika Kivunjo zinaoneshwa katika Jedwali Na. 8 na Na. 9 hapo chini:

**Jedwali Na. 8: Nomino katika Ngeli ya 5 na 6 [i-/ ma-]**

| Na. | Umoja | | | Wingi | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| (a) | i- | wenje | 'mende' | ma- | wenje | 'mende' |
| | KNg | Sh | | KNg | Sh | |
| (b) | i- | pfue | 'nyani' | ma- | pfue | 'nyani' |
| | KNg | Sh | | KNg | Sh | |
| (c) | i- | kunga | 'samaki' | ma- | kunga | 'samaki' |
| | KNg | Sh | | KNg | Sh | |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2013)

Jedwali Na. 8 linaonesha nomino za ngeli ya 5 umoja na 6 wingi. Maneno hayo katika umoja yanaanza na irabu /i/ na katika wingi maneno hayo huanza na silabi (ma). Kwa mfano, katika data iliyotolewa, maneno *i-wenje*, i-pfue na i-kunga umoja na *ma-wenje, ma-pfue na ma-kunga* wingi yamebeba viambishi ngeli i-/ma- ambavyo ni ngeli ya 5 na 6. Data katika Jedwali Na. 9 zinaonesha namna ngeli ya 5 inavyoweza kujitokeza katika umbo tofauti ambalo ni /Ø/:

**Jedwali Na. 9: Nomino katika Ngeli ya 5 na 6 [Ø-/ ma-]**

| Na. | Umoja | | | Wingi | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| (a) | Ø- | fumvu | 'msitu' | ma- | fumvu | 'misitu' |
| | KNg | Sh | | KNg | Sh | |
| (b) | Ø- | oṙe | 'jipu' | ma- | oṙe | 'majipu' |
| | KNg | Sh | | KNg | Sh | |
| (c) | Ø- | yewo | 'jino' | ma- | yewo | 'meno' |
| | KNg | Sh | | KNg | Sh | |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2013)

Kwa hiyo, katika lugha ya Kivunjo, ngeli ya 5 inaweza kujitokeza katika maumbo mawili tofauti lakini katika wingi umbo ni moja tu. Katika maneno yaliyotolewa

ambayo ni Ø *fumvu*, *Ø- oṙe* na *Ø-yewo* umoja na *ma-fumvu*, *ma- oṙe* na *ma-yewo* wingi, yamebeba viambishi ngeli, Ø- /ma- ambavyo ni ngeli ya 5 na 6.

#### 4.1.5 Ngeli ya 7 na 8 [ki-shi]

Katika lugha ya Kivunjo, ngeli ya 7 umoja inawakilishwa na kiambishi /ki-/. Katika mazingira maalumu, kiambishi hiki hubadilika na hujitokeza katika alomofu mbili tofauti ambazo ni: {ki-} au {ky-}. Ngeli ya 8 wingi inawakilishwa na kiambishi /shi-/ na kiambishi hiki kina alomofu mbili tofauti ambazo ni: {shi} au {shy}. Nomino katika ngeli ya 7 na 8 katika Kivunjo zinaoneshwa katika Jedwali Na. 10 na Na. 11:

**Jedwali Na. 10: Nomino katika Ngeli ya 7 na 8 [ki-/ shi-]**

| **Na.** | **Umoja** | | | **Wingi** | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| (a) | ki- | kapu | 'kikapu' | shi- | kapu | 'vikapu' |
| | KNg | Sh | | KNg | Sh | |
| (b) | ki- | miyo | 'kidole' | shi- | miyo | 'vidole' |
| | KNg | Sh | | KNg | Sh | |
| (c) | ki- | tara | 'kitanda' | shi- | tara | 'vitanda' |
| | KNg | Sh | | KNg | Sh | |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2013)

Data katika Jedwali Na. 10 zinaonesha mofimu ya ngeli ya 7 umoja /ki-/ na wingi /shi-/. Data hiyo inaonesha kuwa alomofu {ki-} hujitokeza katika mazingira ya kiambishi hicho kufuatiwa na konsonanti. Maneno katika jedwali; *ki-kapu*, *ki-miyo* na *ki-tara* umoja na *shi-kapu*, *shi-miyo* na *shi-tara* wingi yanabeba viambishi ki-/shi- ambavyo ni viambishi ngeli za 7 na 8.

**Jedwali Na. 11: Nomino katika Ngeli ya 7 na 8 [ky-/ shy-]**

| **Na.** | **Umoja** | | | **Wingi** | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| (a) | ky- | ela | 'chakula' | shy- | ela | 'vyakula' |
| | KNg | Sh | | KNg | Sh | |
| (b) | ky- | eri | 'wakati' | shy- | eri | 'wakati' |
| | KNg | Sh | | KNg | Sh | |
| (c) | ky- | aro | 'safari' | shy- | aro | 'safari' |
| | KNg | Sh | | KNg | Sh | |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2013)

Mifano katika Jedwali Na. 11 inaonesha mofimu /ki-/ huwa {ky-} katika mazingira ambapo mzizi wa nomino unaanza na irabu. Pia, mofimu /shi-/ huwa {shy-} katika mazingira ambapo mzizi wa nomino unaanza na irabu. Mabadiliko haya yanajitokeza kwa sababu ya mchakato wa kifonolojia wa uyeyushaji. Kwa mfano, katika Jedwali Na. 11, maneno *ky-ela*, *ky-eri* na *ky-ari* umoja na *shy-ela*, *shy-eri* na

*shy-aro* wingi yamebeba viambishi ky-/shy- ambavyo ni alomofu ya viambishi ngeli ya 7 na 8.

### 4.1.6 Ngeli ya 9 na 10 [n- / n-]

Katika lugha ya Kivunjo, ngeli ya 9 umoja inawakilishwa na kiambishi /n-/. Ngeli ya 10 wingi pia inawakilishwa na kiambishi /n-/. Katika mazingira maalumu, kiambishi ngeli /n-/ kina alomofu tano tofauti ambazo ni: {**n-**}, {**m-**}, { **ŋ-**}, { **ɲ-**} au { **ɱ** -}. Nomino katika ngeli za 10 na 11 katika Kivunjo zinaoneshwa katika Jedwali Na. 12 hadi Jedwali Na. 16:

**Jedwali Na. 12: Nomino katika Ngeli za 9 na 10 [n-/ n-]**

| Na. | Umoja | | | Wingi | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| (a) | n- | daa | 'chawa' | n- | daa | 'chawa' |
| | KNg | Sh | | KNg | Sh | |
| (b) | n- | deu | 'tumbo' | n- | deu | 'tumbo' |
| | KNg | Sh | | KNg | Sh | |
| (c) | n- | denga | 'shida' | n- | denga | 'shida' |
| | KNg | Sh | | KNg | Sh | |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2013)

Jedwali Na. 12 linawasilisha ngeli za 9 na 10 katika umbo lake la asili la kiambishi /n-/ katika umoja na kiambishi /n-/ katika wingi. Viambishi hivi vya umoja na wingi katika ngeli hii hujitokeza pale ambapo mzizi wa nomino umeanza na konsonanti ya ufizi. Katika Jedwali na.12 maneno *n-daa*, *n-deu*, na *n-denga* umoja na wingi yamebeba viambishi *n-/n-* ambavyo ni viambishi ngeli ya 9 na 10.

**Jedwali Na. 13: Nomino katika Ngeli ya 9 na 10 [m-/ m-]**

| Na. | Umoja | | | Wingi | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| (a) | m- | beu | 'mbegu' | m- | beu | 'mbegu' |
| | KNg | Sh | | KNg | Sh | |
| (b) | m- | beta | 'ndege' | m- | beta | 'ndege' |
| | KNg | Sh | | KNg | Sh | |
| (c) | m- | buo | 'pua' | m- | buo | 'pua' |
| | KNg | Sh | | KNg | Sh | |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2013)

Data katika Jedwali Na. 13 inaonesha nomino katika ngeli ya 9 na 10 zikiwa na kiambishi /m-/ katika umoja na /m-/ katika wingi. Alomofu {m-} ya kiambishi /n-/ katika ngeli hii hujitokeza katika mazingira ambapo mzizi wa nomino umeanza na konsonanti ya midomo na hivyo kusababisha nazali /n-/ kubadilika na kuwa nazali ya midomo /m-/.

**Jedwali Na. 14: Nomino katika Ngeli za 9 na 10 [ŋ- / ŋ-]**

| Na. | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| (a) | ŋ- gosi 'ngozi'<br>KNg Sh | ŋ- gosi 'ngozi'<br>KNg Sh |
| (b) | ŋ- gume 'ngumi'<br>KNg Sh | ŋ- gume 'ngumi'<br>KNg Sh |
| (c) | ŋ- goo 'moyo'<br>KNg Sh | ŋ- goo 'moyo'<br>KNg Sh |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2013)

Katika Jedwali Na. 14, data inaonesha kiambishi cha ngeli ya 9 na 10 kikijitokeza katika alomofu {ŋ} katika umbo lake la umoja na wingi. Alomofu hii hujitokeza katika mazingira ambapo mzizi wa nomino umeanza na konsonanti ya kaakaa laini na kusababisha nazali /n-/ kubadilika na kuwa nazali /ŋ/ katika umbo lake la umoja na wingi. Maneno *ŋ-gosi, ŋ-gume* na *ŋ-goo* umoja na wingi katika jedwali na.14 yamebeba viambishi *ŋ- /ŋ-* ambavyo ni alomofu ya viambishi ngeli ya 9 na 10 ambavyo ni *n-/n-*.

**Jedwali Na. 15: Nomino katika Ngeli za 9 na 10 [ɱ- / ɱ-]**

| Na. | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| (a) | ɱ- vuo 'mvua'<br>KNg Sh | ɱ- vuo 'mvua'<br>KNg Sh |
| (b) | ɱ- viao 'laana'<br>KNg Sh | ɱ- viao 'laana'<br>KNg Sh |
| (c) | ɱ- vinyiko 'mfuniko'<br>KNg Sh | ɱ- vinyiko 'mfuniko'<br>KNg Sh |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2013)

Katika Jedwali Na**.** 15, data inaonesha kiambishi cha ngeli za 9 na 10 kikijitokeza kama alomofu /ɱ/ katika umbo lake la umoja na wingi. Alomofu hii hujitokeza katika mazingira ambapo mzizi wa nomino unaanza na konsonanti ya mdomo meno, na kusababisha nazali /n-/ kubadilika na kuwa nazali ya midomo meno / ɱ-/. Kwa mfano, maneno *ɱ-vuo, ɱ-viao* na *ɱ-vinyiko* umoja na wingi katika Jedwali Na.15, yamebeba viambishi ɱ-/ ɱ- ambavyo ni alomofu za viambishi ngeli za 9 na 10 ambavyo ni *n-/n-*.

**Jedwali Na. 16: Nomino katika Ngeli za 9 na 10 [ɲ- / ɲ-]**

| Na. | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| (a) | ɲ- au 'nyau'<br>KNg Sh | ɲ- au 'nyau'<br>KNg Sh |
| (b) | ɲ- ama 'nyama'<br>KNg Sh<br>ɲ- anya 'nyanya' | ɲ- ama 'nyama'<br>KNg Sh<br>ɲ- anya 'nyanya' |

| Na. | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| (c) | KNg Sh | KNg Sh |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2013)

Katika Jedwali Na. 16, data inaonesha kuwa ngeli za 9 na 10 zinaweza kuwakilishwa na alomofu {ɲ-} katika mazingira ambayo kiambishi ngeli cha asili /n-/ kimefuatiwa na konsonanti ya kaakaa gumu na kusababisha nazali /n/ kubadilika na kuwa nazali ya kaakaa gumu. Kwa mfano, katika Jedwali Na. 16, maneno *ɲ-au*, *ɲ-ama* na *ɲ-anya* umoja na wingi yamebeba viambishi *ɲ-/ ɲ-* ambavyo ni alomofu za viambishi ngeli za 9 na 10.

#### 4.1.7 Ngeli za 11 na 10 [u-/ n-]

Katika lugha ya Kivunjo, ngeli ya 11 umoja inawakilishwa na kiambishi ngeli /u-/, lakini katika wingi hakuna kiambishi ngeli kinachowakilisha ngeli hii, hivyo huchukua wingi katika ngeli ya 10 kwa kiambishi ngeli /n-/. Aidha, kiambishi ngeli cha ngeli ya 10 /n-/ wakati mwingine kinapachikwa kwenye nomino pamoja na kiambishi awali cha nomino hizo za ngeli ya 11 na kusababisha alomofu /ngy-/ na /n-/. Wakati mwingine, kiambishi ngeli hiki /n-/ hupachikwa moja kwa moja kwenye mizizi. Zingatia mifano ya nomino katika ngeli za 11 na 10 katika Kivunjo kama zinavyooneshwa katika majedwali Na. 17 na 18:

**Jedwali Na. 17: Nomino katika Ngeli ya 11 na 10 [u-/ n-]**

| Na. | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| (a) | u- rusu 'uzi'<br>KNg Sh | n- ndusu 'nyuzi'<br>KNg Sh |
| (b) | u- jaa 'ukucha'<br>KNg Sh | n- jaa 'kucha'<br>KNg Sh |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2013)

Jedwali Na. 17 linaonesha data za ngeli za 11 na 10 ambapo katika ngeli ya 11 inawakilishwa na kiambishi /u-/ na ngeli ya 10 ambayo ni wingi wake inawakilishwa na kiambishi /n-/ ambacho ni kiambishi ngeli cha ngeli za 9 na 10. Katika jedwali Na.17, maneno *u-rusu*, *u-jaa* ambayo ni umoja na *n-ndusu*, *n-jaa* wingi yamebeba viambishi *u-/n-* ambavyo ni viambishi ngeli ya 11 na 10. Ngeli ya 10 imejitokeza hapa kwa sababu ngeli ya 11 umoja imechukua kiambishi ngeli cha wingi katika ngeli ya 10. Mifano katika Jedwali Na. 18 inafafanua zaidi:

**Jedwali Na. 18: Nomino katika Ngeli ya 11 na 10 [u-/ ngy-]**

| Na. | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| (a) | u- poi 'fimbo ya kutembelea'<br>KNg Sh | ngy- u- poi 'fimbo ya kutembelea'<br>KNg KNg Sh |

| Na. | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| (b) | u- rongo 'ubongo'<br>KNg Sh | ngy- u- rongo 'ubongo'<br>KNg KNg Sh |
| (c) | u- wishi 'mwewe'<br>KNg Sh | ngy- u- wishi 'mwewe'<br>KNg KNg Sh |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2013)

Kama inavyonekana katika Jedwali Na.18, maneno *u-poi, u-rongo,* na *u-wishi* ambayo ni umoja, na *ngy-u-poi, ngy-u-rongo* na *ngy-u-wishi* ambayo ni wingi yamechukua viambishi ngeli *u-/ngy-* vya ngeli ya 11 na 10 ambapo kiambishi ngeli *ngy-* ni alomofu ya kiambishi ngeli *n-*.

#### 4.1.8 Ngeli ya 14 na ya 6 [u- / ma-]

Katika lugha ya Kivunjo, ngeli ya 14 inawakilishwa na kiambishi ngeli /u-/, katika baadhi ya maneno kiyeyusho w- hujitokeza mwanzoni mwa maneno yenye kiambishi ngeli u-. Aidha, ngeli ya 14 huchukua wingi katika ngeli ya 6 kwa kiambishi ngeli /ma-/. Nomino za Kivunjo zilizomo katika ngeli ya 14 zinaoneshwa katika Jedwali Na.19 na Na:

**Jedwali Na. 19: Nomino katika Ngeli ya 14 na ya 6 [u-/ ma-]**

| Na. | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| (a) | u- cha 'uzuri'<br>KNg Sh | ma- cha 'mazuri'<br>KNg Sh |
| (b) | u- wicho 'ubaya'<br>KNg Sh | ma- wicho 'mabaya'<br>KNg Sh |
| (c) | u- ku 'chakavu'<br>KNg Sh | ma- ku 'chakavu'<br>KNg Sh |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2013)

Katika Jedwali Na. 19, data hiyo inaonesha ngeli ya kiambishi ngeli ya 14 ni /u-/ katika umoja katika mazingira maalumu na katika wingi ngeli hiyo inachukua kiambishi cha ngeli ya 6 /ma-/ katika mazingira yote. Kwa mfano, katika Jedwali Na.19, maneno *u-cha, u-wicho,* na *u-ku* ambayo ni umoja na *ma-cha, ma-wicho na ma-ku* ambayo ni wingi yamechukua viambishi ngeli *u-/ma-*ambavyo ni viambishi ngeli za 14 na 6, ambapo kiambishi ngeki ya 14 *u-* ambacho ni umoja kimechukua kiambishi ngeli cha *ma-* katika ngeli ya 6.

**Jedwali Na. 20: Nomino katika Ngeli ya 14 na ya 6**

| Na. | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| (a) | w- u- mangi 'utemi'<br>Mt KNg Sh | w- u- mangi 'utemi'<br>Mt KNg Sh |

| Na. | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| (b) | w- u- ng'anyi 'ukubwa' | w- u- ng'anyi 'ukubwa' |
| | Mt KNg Sh | Mt KNg Sh |
| (c) | w- u- tondo 'ujinga' | w- u- tondo 'ujinga' |
| | Mt KNg Sh | Mt KNg Sh |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2013)

Katika Jedwali Na. 20 hapo juu, Mt inawakilisha mofu tupu[6]. Katika mifano hiyo. utaona kiyeyusho /w-/ kinajitokeza mwanzoni mwa neno na kufuatiwa na kiambishi ngeli /u-/. Kwa mfano, data katika Jedwali Na. 20, maneno *w-u-mangi, w-u-ng'anyi, w-u-tondo* ambayo ni umoja na wingi yametanguliwa na mofu tupu *w-* ambayo haiwakilishi umbo lolote. Mofu *w-* inajitokeza kabla ya kiambishi ngeli ambacho ni *u-*.

### 4.1.9 Ngeli za 15 na ya 6 [ku- / ma-]

Katika lugha ya Kivunjo, ngeli ya 15 inawakilishwa na kiambishi ngeli /ku-/. Ngeli hii ni ya umoja ambayo huchukua wingi katika ngeli ya 6, nomino katika ngeli hii ni chache sana ambazo zinahusu viungo vya mwili. Nomino katika ngeli ya 15 na 6 katika Kivunjo zinaoneshwa katika Jedwali Na. 21:

**Jedwali Na. 21: Nomino katika Ngeli za 15 na ya 6 [ku-/ ma-]**

| Na. | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| (a) | ku- ṙende 'mguu' | ma- ṙende 'miguu' |
| | KNg Sh | KNg Sh |
| (b) | ku- woko 'mkono' | ku- woko 'mkono' |
| | KNg Sh | KNg Sh |
| (c) | ku- ṙu 'sikio' | ma- ṙu 'masikio' |
| | KNg Sh | KNg Sh |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2013)

Katika Jedwali Na. 21, data inaonesha kuwa ngeli ya 15 /ku-/ umoja inachukua kiambishi ngeli ya 6 /ma-/ katika wingi. Kwa mfano, maneno *ku- ṙende***,** *ku-woko* na *ku-ṙu* ambayo ni umoja na *ma- ṙende***,** *ma-woko* na *ma-ṙu* ambayo ni wingi yamebeba viambishi *ku-/ma-* ambavyo ni viambishi ngeli ya 15 na 6. Hata hivyo, kiambishi cha ngeli ya 15 umoja kimebeba kiambishi ngeli cha wingi katika ngeli ya 6.

### 4.1.10 Ngeli ya 15a [i-]

Katika lugha ya Kivunjo, ngeli ya 15a hubeba nomino zilizoundwa kutokana na

[6] Mofu tupu ni umbo ambalo haliwakilishi mofimu yoyote.

vitenzi. Mizizi ya vitenzi hivyo vikiambikwa kiambishi /i-/ hupata hadhi ya kuwa nomino. Nomino katika ngeli ya 15(a) katika Kivunjo zinaoneshwa katika Jedwali Na. 22:

**Jedwali Na. 22: Nomino katika ngeli ya 15a [i-]**

| Na. | Nomino | | |
|---|---|---|---|
| (a) | i- | ṙema | 'kulima' |
| | KNg | Sh | |
| (b) | i- | tema | 'kucheza' |
| | KNg | Sh | |
| (c) | i- | iimba | 'kuimba' |
| | KNg | Sh | |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2013)

Katika Jedwali Na. 22, data inaonesha kuwa katika lugha ya Kivunjo kuna nomino ambazo zimeundwa kwa mchakato wa unominishaji ambapo kitenzi huwekewa irabu /i-/ mwanzoni na kuwa kitenzi jina. Kwa mfano, katika Jedwali Na. 22, maneno *i-ṙema, i-tema* na *i-iimba* ni vitenzi ambavyo vimewekewa kiambishi *i-* na kuvifanya kuwa vitenzi jina.

**4.1.11 Ngeli ya 16, 17 na 18 [pa-/hu-/mu-]**

Ngeli ya 16, 17 na 18 katika Kivunjo hubeba nomino za mahali. Nomino hizi zimegawanyika katika makundi makuu mawili. Kwa mujibu wa Nchimbi (2004), makundi hayo ni nomino za mahali si tegemezi, yaani zinazojitegemea[7] na nomino za mahali tegemezi[8]. Kwa hiyo, katika Kivunjo, ngeli ya 16 inawakilishwa na kiambishi ngeli /ha-/, ngeli ya 17 inawakilishwa na kiambishi ngeli /ku-/ na ngeli ya 18 inawakilishwa na kiambishi /-nyi/. Mofimu zote hizi tatu hazina alomofu. Nomino katika ngeli ya 16, 17 na 18 katika Kivunjo zinaoneshwa katika Jedwali Na. 23 na Na. 24 hapo chini: Mfano (i) ni kwa ajili ya nomino za mahali zinazojitegemea na Mfano (ii) ni kwa ajili ya nomino tegemezi.

**Jedwali Na. 23: Nomino za Mahali Zinazojitegemea za Ngeli ya 16 na 17**

| Na. | Kng. | Mifano | | |
|---|---|---|---|---|
| (i) | ha- | ha- | la | 'pale' |
| | | KNg | Sh | |
| (ii) | ku- | ku- | la | 'kule' |
| | | KNg | Sh | |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2013)

Data imeonesha katika Jedwali Na. 23 kuwa katika lugha ya Kivunjo nomino za

[7] Zinaweza kusimama zenyewe kuonesha mahali na kuleta maana.

[8] Haziwezi kusimama peke yake kuonesha mahali na kuleta maana.

mahali za msingi ni; *hala 'pale' na kula 'kule'*. Maneno ha-la na ku-la yamebeba viambishi ngeli *ha-/ku-* ambavyo ni viambishi ngeli ya mahali ya 16 na 17.


**Jedwali Na. 24: Nomino za Mahali Tegemezi za Ngeli ya 16, 17 na 18**

| Na. | Kng | Nomino | |
|---|---|---|---|
| **16** | ha- | ha- fanyi<br>KNg Sh | 'pachafu' |
| **17** | ku- | ku- oṙe<br>KNg Sh | 'kuna' |
| **18** | -nyi | mawoko -nyi<br>Sh KNg | 'mikononi' |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2013)

Mfano katika Jedwali na.24 unaonesha dhahiri nomino za mahali fuatizi huundwa kutokana na nomino ambazo asili yake sio nomino za mahali bali ni za ngeli nyingine, lakini nomino hizo zikiambikwa viambishi vya ngeli vya mahali huleta dhana ya mahali. Kwa mfano, maneno *ha-fanyi, ku- oṙe* na *mawoko-nyi* yamebeba viambishi *ha-/ku-/-nyi* ambavyo vikipachikwa kwenye neno lolote vinaleta dhana ya mahali. Kiambishi *–nyi* huwa kinapachikwa mwishoni mwa neno kama kilivyo kiambishi *–ni* katika lugha ya Kiswahili.

Kwa ujumla, huo ndiyo uchambuzi wa ngeli za lugha ya kivunjo kwa kutumia mkabala wa viambishi awali vya nomino, ambapo imebainika kuwa lugha ya Kivunjo ina idadi ya ngeli 18. Hata hivyo, baadhi ya nomino katika lugha ya Kivunjo zina maumbo ya umoja na wingi, na baadhi hazina maumbo ya umoja na wingi. Hivyo, ngeli nyingine zipo katika jozi na nyingine hazipo katika jozi. Hali hii inaoneshwa katika kielelezo Na. 1 hapo chini:




**Kielelezo Na. 1**: Uhusiano wa Viambishi Ngeli vya Umoja na Wingi katika Lugha ya Kivunjo

Kielelezo hiki kinaonesha kuwa, nomino zenye maumbo ya umoja na wingi, ngeli

zake zinaweza kupangwa kwenye jozi zifuatazo: 1/2, 3/4, 5/6, 7/8, 11/10, 15/6, 14/6 na 14/10. Nomino ambazo haziwezi kupangwa katika jozi ya umoja na wingi ziko kwenye ngeli ya 9, 15a, 16, na 17.

**5.0 Hitimisho**

Utafiti huu ulilenga kuchunguza uainishaji wa ngeli za nomino katika lugha ya Kivunjo kwa kutumia Mkabala wa Kimofolojia. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kwamba viambishi ngeli vimebainishwa kwa kutenga viambishi vya nomino vya umoja na wingi kuwa katika ngeli tofauti kwa kutumia Mkabala wa Viambishi Awali vya Nomino. Uainishaji huu umetupatia ngeli 18, kama zilivyooneshwa katika jedwali Na. 1.

**Marejeleo**


Ashton, E.O. (1944). *Swahili Grammar: Including Intonation.* London: Longman Group Ltd.

Besha, R.M. (1985). *A Study of Tense and Aspects in Shambala*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Bleek, W.H.I. (1862). A *Comparative Grammar of South African Languages*. London: Trubner Co.

Dressler, W.U. (1985). "On the Predictiveness of Natural Morphology". *Journal of Linguistics.* 21: 321-338.

Elisifa, Z.S. (2008). *Motisha katika Ujifunzaji Kiswahili kama Lugha ya Pili*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

John, B. (2011). *Nafasi ya Viarudhi katika Lugha ya Kivunjo: Uamilifu wa Toni katika Irabu Ndefu na Fupi*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kahigi, K.K. (2005). "The Sisumbwa Noun: It's Classes and Derivation." *Occasional Paper in Linguistics.* 1:117-154.

Kapinga, M.C. (1983). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu.* Dar es Salaam: TUKI.

Katushemererwe, F. na Hanneforth, T. (2010). The Morphological Analysis of Bantu Nouns-First Experiences from Runyakitara. *Nordic Journal of African Studies*. 19(1): 1-22.

Kihore, Y.M., Massamba, D.P.B., na Msanjila, Y.P. (2003). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA): Sekondari na Vyuo*. TUKI

Kombe, L.E. (2010). *The Formation of Relative Clauses in Kivunjo*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Maho, J. (1999). *A Comparative Study of Bantu Noun Classes*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Goteborg University.

Makule, A.O. (2006). *Mofimu Kanushi katika lahaja ya Kivunjo*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Massamba, D.P.B. (1995). "The Classification of Ci-Ruri Nouns". *Journal of Asia and African Studies*. 48: 605-629.

Mutaka, N. na Tamanji, P.N. (2000). *Introduction to African Linguistics.* Muenchen: Lincom Handbooks in Linguistics.

Mwendamseke, F.J. (2011). *Uainishaji wa Ngeli za Nomino katika Lugha ya Kibena*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Petzell, M. (2008). *The Kagulu Language of Tanzania Grammar, Texts, and Vocabulary*. Cologne: Rüdiger Köppe Verlag.

Polome, E.C. (1976). *Swahili Language Handbook*. Washington D.C: Center for Applied Linguistics.

Rugemalira, M.J. (2005). *A Grammar of Runyambo.* University of Dar es Salaam: LOT.